

---

Ghorofa ya 7, Jengo la LAMP Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama  
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

---

## **TANGAZO KWA UMMA**

### **MWITO WA KUPATA MAONI KUHUSU MAPITIO YA KANUNI YA KUKOKOTOA BEI ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI (*PETROLEUM PRODUCTS*)**

MAMLAKA ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea hoja kutoka kwa wadau wa sekta ya mafuta kuhusu mambo mawili: (i) Umuhimu wa kuangalia upya kiasi cha tozo inayotozwa na TIPER (*TIPER fee*) kwa kampuni za kuuza mafuta kwa jumla (*Oil Marketing Companies "OMCs"*), kutumia *manifold* ya kampuni hiyo kwa ajili ya kupokea mafuta ya petroli (*petroleum products*) (ii) Kutojumuishwa kwa tozo mbalimbali katika kanuni ya kukokotoa bei za bidhaa za mafuta zinazolipwa na wafanyabiashara wanaoendesha vituo vya kuuza mafuta kwa rejareja (*Retailers*). Tozo hizo ni zile zinazolipwa kwa halmashauri na taasisi za serikali ikiwamo Wakala wa Vipimo (WMA), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na Ofisi za Zimamoto na Uokoaji za Mikoa. Taarifa za kuthibitisha hoja ya *Retailers* kuhusu malipo ya tozo kwa halmashauri na taasisi za serikali zimewasilishwa EWURA.

Baada ya kuzifanyia uchambuzi taarifa hizo, EWURA inapendekeza mapitio mapya ya Kanuni ya Kukokotoa Bei za Bidhaa za Mafuta. Mapitio hayo yatahakikisha tozo inayotozwa na TIPER ni stahiki na pia tozo zinazolipwa na *Retailers* kwa ajili ya kufanya malipo kwa halmashauri na taasisi za serikali zinazingatiwa, ikiwa ni pamoja na kuzitofautisha tozo hizo kati ya *OMCs* na *Retailers*.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 19 (2)(b) cha Sheria ya EWURA Na. 414, EWURA inaanzisha mchakato wa kupata maoni ya wadau kuhusiana na pendekezo la kufanya mapitio ya Kanuni ya Kukokotoa Bei za Bidhaa za Mafuta ili kuhakikisha kwamba tozo ya TIPER ni stahiki kulingana na gharama halisi ya uendeshaji wa *manifold* yake na pia kuweka tozo halisi kwa ajili ya malipo kwa halmashauri na taasisi za serikali zinazolipwa na Kampuni za Kuuza Mafuta kwa jumla na. katika mchakato huo, EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na *OMCs*; *Retailers*; Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) na mabaraza ya halmashauri na wananchi.

Mkutano wa Taftishi wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau utafanyika tarehe **14 Septemba 2016** katika Ofisi za EWURA za Dar es Salaam kuanzia saa nne asubuhi.

Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe 21 Septemba 2016. Wadau watakaopenda kupewa muda wa kuwasilisha maoni yao katika mkutano wa wadau wanatakiwa kuonesha nia yao kwa kuiandikia EWURA ifikapo tarehe **13 Septemba 2016**.

Mamlaka imeandaa Muhtasari wa Majadiliano kuhusiana na mada hii. Nakala za Muhtasari huu zinapatikana katika ofisi za Mamlaka wakati wa muda wa kazi kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa wa kutoa maoni yao ili kufanikisha zoezi hili. Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo juu.

**Limetolewa na:**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**